



Utafiti na Uchanganuzi wa Usawa wa Nauli katika Mfumo Mzima wa RTD

RTD ni mtoa huduma wa usafiri wa umma katika jiji la Denver. Kwa kujibu maoni kutoka kwa wateja wanaosema kwamba nauli ni ghali na zinachanganya, RTD ilianzisha Utafiti na Uchanganuzi wa Usawa wa Nauli katika Mfumo Mzima ili kuzifanya nauli kuwa zenye **usawa**, **nafuu** na **rahisi** zaidi. Angalia mabadiliko ambayo RTD inapendekeza kufanyia nauli zake!

Mapendekezo ya Utafiti wa Nauli

Muundo Mpya Kamili wa Nauli

Muundo kamili wa nauli uliopendekezwa **unapunguza nauli kwa wateja wote** na **unaondoa nauli za Kimaeneo**.

	NAULI KAMILI ZA SASA			NAULI KAMILI ZINAZOPENDEKEZWA	
	Mtaa	Kieneo	Uwanja wa Ndege	Kiwango (Mtaa/Kieneo)	Uwanja wa Ndege (SkyRide/A Line)
Saa 3	\$3.00	\$5.25	\$10.50	\$2.75	\$10
Siku	\$6.00	\$10.50		\$5.50	
Kila Mwezi	\$114	\$200		\$88	

- Safari kuelekea na kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Denver (kwa kutumia A Line au SkyRide) itagharimu \$10
- Safari nyingine zote katika eneo la huduma la RTD zitagharimu \$2.75 kwa Pasi ya Saa 3 au \$5.50 kwa Pasi ya Siku Nzima
- Wateja wa Pasi ya Kila Mwezi watasafiri popote, ikiwa ni pamoja na kuenda na kutoka kwenye uwanja wa ndege kwa \$88

Muundo Mpya wa Nauli ya Punguzo

RTD ina nauli za punguzo kwa watu wazima wa umri wa miaka 65 na zaidi, watu binafsi wenye ulemavu, wapokeaji wa Medicare na watu binafsi walio na mapato ya chini ("LiVE"). Mfumo wa nauli ya Punguzo unaopendekezwa **unapunguza nauli kwa wateja wa Punguzo** na **unaweka pamoja nauli zote** ili **watu wote wazima wanaotumia nauli za Punguzo walipe bei sawa kwa safari yoyote**.

	NAULI ZA SASA ZA PUNGUZO <i>Umri wa miaka zaidi ya 65, ulemavu, nauli za wapokeaji wa Medicare / nauli za LiVE</i>			NAULI ZA PUNGUZO ZINAZOPENDEKEZWA
	Mtaa	Kieneo	Uwanja wa Ndege	Mtaa, Kieneo na Uwanja wa Ndege
Saa 3	\$1.50 / \$1.80	\$2.60 / \$3.15	\$10.50 / \$6.30	\$1.35
Siku	\$3.00 / \$3.60	\$5.25 / \$6.30		\$2.70
Kila Mwezi	\$57 / \$68.40	\$99 / \$119.70		\$27



- Watu wazima wanaotumia nauli za Punguzo wanaweza kusafiri *mahali popote*, ikiwa ni pamoja na uwanja wa ndege, kwa bei ya nauli ya Punguzo
 - Pasi ya Saa 3 itagharimu \$1.35 na Pasi ya Siku itagharimu \$2.70 (Punguzo la asilimia 50 la nauli Kamili)
 - Pasi ya Kila Mwezi itagharimu \$27 (Punguzo la asilimia 70 la nauli Kamili)

Upanuzi wa Mpango wa Punguzo Kulingana na Mapato wa LiVE (LiVE Income-Based Discount Program Expansion)

Wateja zaidi walio na mapato ya chini watastahiki mpango wa punguzo kulingana na mapato wa LiVE chini ya pendekezo. RTD inapendekeza:

- Kuondoa matakwa ya sasa ya kuwa na anwani ndani ya mipaka ya RTD
- Kuongeza vigezo vya mapato ya kaya kwa ustahiki wa punguzo wa LiVE. Chini ya pendekezo jipya, familia ya watu wanne inaweza kupata mapato ya kaya ya \$75,000 au chini na kustahiki punguzo la LiVE

Wateja wa Access-a-Ride pia watastahiki nauli za Access-a-Ride za punguzo la LiVE.

Mipango ya Vijana na Wanafunzi

Pendekezo linawezesha usafiri kuwa nafuu zaidi kwa vijana na wanafunzi pia.

- Watoto wote wa umri wa miaka 5 au chini tayari husafiri bila malipo wakiandamana na mtu mzima anayelipa nauli (kikomo ni watoto 3 kwa kila mtu mzima)
- Vijana walio na umri wa miaka 19 na chini watasafiri bila malipo chini ya mpango wa jaribio wa mwaka mmoja wa Zero Fares for Youth
- Wanafunzi walio kwenye vyuo vya jamii vinavyoshiriki, shule za kiufundi au vyo na vyuo vikuu vingine ambao hawajajiandikisha katika CollegePass watastahiki SemesterPass ya \$70 kwa mwezi



Je, unataka RTD iyafanye mapendekezo haya yawe rasmi?

Toa maoni yako kupitia barua pepe dani.mclean@rtd-denver.com kufikia tarehe 22 Mei, au pata maelezo zaidi kwa kuhudhuria tukio au kwa kutembelea farefeedback.rtd-denver.com. **Huduma za tafsiri na ukalimani zinapatikana kwa kutuma ombi.**